






# Nozibebe na nywele tatu

-  Tessa Welch
-  Wiehan de Jager
-  Matteo E. Mwita
-  Kiswahili
-  Level 3

(imageless edition)







Hapo zamani za kale, wasichana watatu walienda kukusanya kuni.



Ilikuwa ni siku yenye jua kali na wakaamua kwenda mtoni kuogelea. Wakaogelea huku wakicheza na kurushiana maji.



Ghafa waligundua kuwa muda  
umekwenda. Wakaharakisha kurudi  
nyumbani.




Walipokuwa wanakaribia kufika nyumbani, Nozibele akajishika shingoni. Alikuwa amesahau shanga zake! “Tafadhali turudini!” aliwasihi rafiki zake. Lakini rafiki zake wakasema tumechelewa.



Kwa hiyo Nozibele akarudi mwenyewe mtoni. Akapata shanga zake na akakimbia kurudi nyumbani. Lakini akapotea gizani.




Kwa mbali akaona mwanga unatoka kwenye nyumba. Akakimbilia kwenye nyumba na kugonga mlango.




Akastaajabu kumwona mbwa  
akifungua mlango na akasema,  
“Unataka nini?” “Nimepotea na  
ninatafuta sehemu ya kulala,” akasema  
Nozibele. “Ingia ndani, la sivyo  
nitakung’ata!” mbwa akamwambia.  
Nozibele akaingia ndani.




Mbwa akamwambia, “Nipikie!”  
“Sijawahi kumpikia mbwa,” akajibu.  
“Pika, la sivyo nitakung’ata!” mbwa  
akasema. Nozibele akampikia mbwa  
chakula.




Mbwa akamwambia, “Nitandikie kitanda!” Nozibele akajibu, “Sijawahi kumtandikia mbwa kitanda.” “Tandika kitanda, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akasema. Nozibele akatandika kitanda.




Akawa kila siku anampikia, anamfulia na kumfagilia mbwa. Siku moja mbwa akasema, “Nozibele, leo naenda kuwatembelea rafiki zangu. Fagia nyumba, pika chakula na osha vitu vyangu kabla sizarudi.”




Mara baada tu ya mbwa kuondoka,  
Nozibele akanyofoa nywele tatu kutoka  
kwenye kichwa chake. Akaweka  
unywele mmoja chini ya kitanda,  
mmoja nyuma ya mlango, na mwingine  
akauweka kwenye uzio wa nyumba.  
Halafu, akakimbia kuelekea nyumbani  
kwa nguvu zote.



Mbwa aliporudi akaanza kumtafuta Nozibele. “Nozibele, uko wapi?” akapiga kelele. “Niko hapa, chini ya kitanda,” unywele wa kwanza ukajibu. “Nipo hapa nyuma ya mlango,” unywele wa pili ukajibu. “Niko hapa kwenye uzio,” unywele wa tatu ukajibu.



Mbwa akagundua kuwa Nozibele amemkimbia. Kwa hiyo akakimbia kuelekea kijijini. Kaka zake Nozibele walikuwa wakimsubiri na fimbo. Mbwa alipowaona akageuka na kukimbia, na hajawahi kuonekana tena.



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

## Nozibele na nywele tatu

Written by: Tessa Welch

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](http://Storybooks Canada) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).